



# Mahitaji ya kuomba viza yako ya Kibinadamu kutoka nje ya Nchi

Ombi lako la viza ya Kibinadamu kutoka nje ya nchi linaendelea kushughulikiwa. Kuendeleza ombi lako utahitajika kufanya tathmini ya matibabu na unaweza pia ukahitaji kuchukuliwa vipimo vya kibiolojia, kwa mfano, alama za vidole.

Serikali ya Australia, kupitia Idara ya Masuala ya Ndani ya Nchi, imeteua Toll Transport Pty Ltd (Toll) kama mkandarasi wake wa Huduma ya Msaada wa Uhamiaji, Matibabu na Huduma Husika kwenye programu ya Kibinadamu kwa walio Nje ya Nchi.

Msimamizi wako wa kesi wa Toll atawasiliana nawe ili kukusaidia kupanga siku ya kwenda kwenye uchunguzi wako wa matibabu na ukusanyaji wa bayometriki.

Ikiwa umetuma ombi la mojawapo ya viza ifuatavyo ya Kibinadamu ya nje ya Nchi;

- Mkimbizi (daraja 200)
- Usaidizi Maalum wa Kibinadamu ndani ya nchi (daraja 201)
- Uokoaji wa Dharura (daraja 203) au
- Mwanamke aliye hatarini (daraja 204)

Gharama za uchunguzi wa kimatibabu, ukusanyaji wa biolojia (ikihitajika), usafiri Kwenda kufanya vipimo, na malazi yoyoye yatakayohitajika yatalipwa na idara.

Iwapo umetuma ombi la Msaidizi Maalum wa Kibinadamu (daraja 202), idara italipa gharama za usafiri za kuhudhuria siku ya kwenda ya matibabu na kibiolojia, (gharama ya ukusanyaji wa kibiolojia itahitaji kulipwa na wewe au mpendekezaji wako). Kama utahitaji kufanya vipimo vya DNA, gharama zozote za usafiri, malazi na ya upimaji wa DNA hautalipiwa na idara na inabidi ujilipie au mpendekezaji (proposer) wako akulipie. Vile vile, gharama za wasindikizaji wa matibabu, kama wanahitajika, inabidi ujilipie au mpendekezaji (proposer) wako akulipie.

Tafadhali hakikisha kwamba unakamilisha ukaguzi wowote ulioombwa ili kuendeleza ombi lako.